**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA TAREHE 18/12/2021**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Charles M. Kazungu | Diwani Butobela | Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. John P. Wanga | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 3. | Mh. Hadija S. Joseph | Diwani Nyamigota | Mjumbe |
| 4. | Mh. Alexander G. Buteyeye | Diwani Lubanga | Mjumbe |
| 5. | Mh. Anthonia Charles | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 6. | Mh. Selemani Gamala | Diwani Busanda | Mjumbe |
| 7. | Mh. Maweda J. Gwesandili | Diwani Isulwabutundwe | Mjumbe |
| 8. | Mh. Elisha H. Lupunga | Diwani Bugulula | Mjumbe |
| 9. | Mh. Malimi S. Saguda | Diwani Nyaruyeye | Mjumbe |
| 10. | Mh. Kulwa L. Giliku | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 11. | Mh. Roza M. Kwiligwa | Diwani Nyachiluluma | Mjumbe |

**WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mh. Tumaini Magesa | Mbunge Jimbo la Busanda kwa taarifa |
| 2. | Mh. Joseph Musukuma | Mbunge Jimbo la Geita kwa taarifa |

**WATAALAMU WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Bless D. Mwakyusa | Afisa Utumishi (W) |
| 2. | Ndg. Hellen Eustace | Afisa Mazingira (W) |
| 3. | Ndg. January Masele | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 4. | Ndg. Hongera Edward | Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 5. | Ndg. Joash Kunaga | Afisa Ugavi (W) |
| 6. | Dkt. Modest Buchard | Mganga Mkuu (W) |



CamScanner

7. Ndg. Mick Chotta — Kaimu Afisa Sheria (W)
8. Ndg. Patricia Nsinde — Mratibu wa UKIMWI (W)
9. Ndg. Richard Mwakihaba — Afisa Elimu Sekondari (W)
10. Ndg. Damian Aloyce — T.E.O - Katoro
11. Ndg. Jackson Felix — Mhasibu wa mapato
12. Ndg. Edith Mpinzile — Afisa Elimu Msingi (W)
13. Ndg. Sarah Yohana — Afisa Mipango (W)
14. Ndg. Thomas Noni — Kaimu Afisa TEHAMA (W)
15. Ndg. Richard kapyela — KaimuAfisa Kilimo Ushirika na Umwagiliaji (W)
16. Ndg. Furaha Chiwile — Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
17. Ndg. Rumoka Buholela — Mweka Hazina (W)
18. Eng. Khamisi Ngonde — Mhandisi wa Ujenzi
19. Ndg. January Bikuba — Afisa Uchaguzi (W)
20. Ndg. Samwel Msongwe — Afisa Biashara
21. Ndg. Fatuma Nassoro — Mwandishi wa Vikao

**KUMB NA. 1/5/12/2021: KUFUNGUA KIKAO:**

Baada ya akidi kutimia, Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Alifungua kikao saa 3:43 asubuhi, akiwaomba wajumbe kuwa huru kujadili ajenda za kikao.

**KUMB NA. 2/5/11/2021: KUTHIBITISHA AJENDA YA KIKAO:**

Wajumbe walithibitisha na kujadili dondoo zifuatazo:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha dondoo za ajenda ya kikao
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 24/11/2021
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 24/11/2021
5. Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2021.
6. Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tsh. 660,972,391.30 kwa ajili ya shughuli za afya kwa mpango wa maendeleo kwa ustawi na mapambano dhidi ya UVIKO-19

3. Ruzuku ya Matumizi mengineyo........................................Tsh. 976,220,950.28
4. Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo........................................Tsh. 10,779,804,024.86

**Jumla Kuu........................................................ Tsh. 32,369,773,789.07**

Kwa upande wa matumizi Mweka Hazina (W) alieleza kwamba Halmashauri kwa kipindi husika imeweza kutumia **Tsh. 24,200,410,341.93** kama inavyoonekana kwenye mchanganua hapa chini:-

1. Matumizi tokana na vyanzo vya ndani kawaida...............Tsh. 758,119,061.00
2. Matumizi tokana na vyanzo vya ndani maendeleo..........Tsh. 871,156,100.00
3. Ruzuku ya Mishahara........................................................Tsh. 18,358,772,000.00
4. Ruzuku ya Matumizi mengineyo......................................Tsh. 1,663,311,890.00
5. Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo......................................Tsh. 2,549,051,260.93

**Jumla kuu...................................................Tsh. 24,200,410,341.93**

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na katika majadiliano yafuatayo yalijitokeza:-

I. Wajumbe walitaka kufahamu hali ya ukusanyaji wa mapato ili kufikia lengo la Halmashauri kwa mwaka, ambapo ilielezwa kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato hauko chini sana kwani hadi kufikia tarehe 30 Novemba 2021 Halmashauri imefikia asilimia 48 ya ukusanyaji mapato;
II. Wajumbe walishauri Kata zote ambazo kwenye taarifa zinaonesha hazijakusanya mapato, mfano; Butobela, Bukondo, Izumacheli, Kagu na zinginezo zifuatiliwe kuona kuna changamoto gani ya ukusanyaji wa Mapato;
III. Wajumbe walishauri baada ya mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa ya UVIKO-19 nguvu kubwa na kasi iliyotumika iendelee na itumike katika ukusanyaji wa mapato; na
IV. Kuhusu fedha ya miradi inayowekwa kwenye akaunti za Kata na Vijiji, wajumbe walielekeza Menejimenti kuandika barua kwa Watendaji wa Kata na Vijiji juu ya fedha iliyoingizwa kwenye akaunti na waheshimiwa madiwani wapatiwe nakala.



CamScanner

7. Malipo ya ongezeko la kazi jengo la utawala Makao Makuu ya Halmashauri.
8. Mapendekezo ya gharama za utekelezaji wa zoezi la uhakiki wa mali za kudumu (Fixed assets Verification) Tshs. 27,750,000.00
9. Maombi ya kupata walinzi kwenye kampuni ya ulinzi
10. maombi ya mabadiliko ya matumizi ya fedha za ndani zitumike kwenye ujenzi wa vyoo shule 2 shikizi
11. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
12. Kufunga kikao

**KUMB NA. 3/5/12/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 24/11/2021:**

Muhtasari wa kikao cha tarehe 02/11/2021 ulisomwa, ukapokelewa kisha ukathibitishwa na kusainiwa.

**KUMB NA. 4/5/12/2021: YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 24/11/2021:**

Katika kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kikao kilichopita yafuatayo yalijitokeza:-

Kuhusu ujenzi wa kivuko cha muda cha izumacheli wajumbe walikadilia kiasi cha Tsh. 5,000,000 lakini kwa sasa imeletwa gharama ya Tsh. 21,846336.5, je kabla ya kufanya tathimini hiyo wataalam wamefatilia maeneo mengine wamefanyaje ili waweze kupata uzoefu. Ambapo ilielezwa kuwa baadhi ya maeneo kuna maegesho ya meli kubwa hivyo boti hizo zinatia nanga kwenye maegesho hayo, Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuomba ujenzi uanze mara moja ili wananchi wapatiwe huduma

**KUMB NA. 5/5/12/2021: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI NOVEMBA, 2021**

Mweka Hazina (W) alisoma na kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba, 2021 ikionesha kuwa Halmashauri imeweza kukusanya jumla ya **Tsh. 32,369,773,789.07** kama inavyoonekana katika mchanganuo ufuatao:-

1. Mapato tokana na vyanzo vya ndani..............................Tsh. 2,254,978,813.46
2. Ruzuku ya Mishahara.....................................................Tsh. 18,358,772,000.00



CamScanner

**KUMB NA. 6/5/12/2021; TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSH. 7,780,972,391.20 KWA AJILI YA SHUGHULI ZA AFYA KWA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19**

Afisa Mipango (W) aliwasilisha taarifa husika akieleza kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilipokea jumla ya Tsh. 7,120,000.000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa madarasa ya shule za Sekondari, shule shikizi na ujenzi wa bweni kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum.

Hivi karibuni katika awamu nyingine Serikali imetoa fedha Tshs. 660,927,391.30 kwa ajli ya shughuli za afya kwa mchanganuo ufuatao:-

- Ujenzi wa jengo la dharula (EMD) Hospitali ya Katoro Tshs. 300,000,000
- Ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) Hospitali ya Nzera Tshs. 250,000,000
- Ujenzi wa nyumba ya mtumishi Hospitali ya Nzera Tshs. 90,000,000
- Fedha kwa ajili ya huduma ya Mkoba wa chanjo Tshs. 18,720,000
- Fedha za uhamasishaji kutumia kutumia PA system Tshs. 2,217,391.30

Wajumbe walipokea taarifa na katika majadiliano walitaka kufahamu mgawanyo wa fedha hiyo na maeneo yaliyopelekewa fedha kama umefanyika. Ambapo ilielezwa ni maelekezo kutoka ofisi ya Rais TAMISEMI. Wajumbe walipitisha taarifa hiyo na kushauri miradi iliyowekewa fedha hiyo kazi ifanyike kwa ufanisi na kwa kasi ile ile kama iliyotumika katika ujenzi wa vyumba vya madarasa ya UVIKO 19.

**KUMB NA. 7/5/12/2021; MALIPO YA ONGEZEKO LA KAZI JENGO LA UTAWALA MAKAO MAKUU YA HALMASHAURI.**

Afisa Mipango (W) aliwasilisha taarifa akieleza kuwa jengo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita linajengwa na mzabuni SUMA JKT. Katika awamu ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. 1,000,000,000 kwa ajili ya kununua vifaa na kumlipa fundi kwa mujibu wa mpango kazi ,fedha ilitarajiwa kufanya kazi zifuatazo:-

- Kujenga msingi
- Nguzo wima (columns)
- Nguzo mlalo (Beams)
- Jamvi la chini na juu
- Ngazi



CamScanner

- Kuezeka

Hata hivyo, gharama zilizopangwa kutumika kujenga msingi wa jengo hilo kwa makadirio ya awali ilikua Tshs. 65,193,760, wakati wa utekelezaji Mzabuni alibaini kuwa vipimo vilivyo ainishwa katika BOQ havikulingana na hali halisi hivyo kusababisha ongezeko la kazi.

Kutokana na ongezeko la kazi gharama zilizopangwa zimeongezeka kutoka Tshs. 65,193,760 ya awali na kufikia Tshs. 95,076,300. Hivyo, Timu ya Menejimenti inaomba idhini ya kufanya ongezeko la Tshs. 29,882,540 kutoka makadirio ya awali.

Wajumbe walipokea taarifa na katika majadiliano yafuatayo yalijitokeza:-

Wajumbe walitaka kufahamu ongezeko la kiasi hicho cha fedha kitalipwa kutoka katika chanzo kipi cha fedha, Ambapo ilielezwa kuwa kiasi hicho kitalipwa kutoka fedha ya mradi (Serikali kuu).

Vile vile, wajumbe walitaka kufahamu utaratibu uliopitiwa na kubaini ongezeko la kazi, Ambapo ilielezwa utaratibu wote wa kisheria umefuatwa kwa kufanya vikao na vielelezo vyote vipo.

Aidha, wajumbe walishauri kabla ya taratibu zingine kuendelea Makamu Mwenyekiti apitie vielelezo vyote vinavyotakiwa kabla ya kufanya malipo ya ongezeko la kazi kama taratibu zimefuatwa na kisha aruhusu taratibu za malipo ziendelee.

**KUMB NA. 8/5/12/2021 MAPENDEKEZO YA GHARAMA ZA UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA UHAKIKI MALI ZA KUDUMU (FIXED ASSETS VERIFICATION) TSHS. 27,750,000.00**

Mweka Hazina (W) aliwasilisha mapendekezo ya gharama na timu zitakazohusika na zoezi la uhakiki wa mali za kudumu (Fixed Assets Verification) zilizopo kwenye jengo la Makao Makuu, Shule za Msingi 211, Sekondari 44, Hospitali 2, Vituo vya Afya 5, Zahanati 39, Ofisi za Serikali za Vijiji 145 na Ofisi za Kata 37 na kuleta jumla ya vituo 484 vitakavyofanyiwa kazi. Zoezi hili litafanyika ndani ya siku 25 kwa kila timu ikiwa ni

wastani wa vituo 9 kwa siku vinavyo patikana kwenye Kata moja au mbili na mchanganuo wa gharama umeonyeshwa kwa timu zote 3.

Wajumbe walipokea taarifa na katika majadiliano yafuatayo yalijitokeza:-

Wajumbe walitaka kufahamu uhakiki wa mali za kudumu unalenga mali zipi na hili ni suala la kisheria au Halmashauri inaamua, Menejimenti ilieleza kuwa suala hili ni hitaji la kisheria, ambapo rasilimali yoyote inayotumika ni lazima ihakikiwe ili kupata thamani halisi ya rasilimali inayotumika, hivyo zoezi la uhakiki ni la Nchi nzima na si kwa Halmashauri hii tu.

**KUMB NA. 9/5/12/2021: MAOMBI YA KUPATA WALINZI KWENYE KAMPUNI YA ULINZI**

Afisa Utumishi (W) aliwasilisha taarifa ya maombi ya kupata walinzi akieleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa vituo vya Afya Bugalama na Ibisabageni. Ili kuhakikisha usalama wa vifaa vya ujenzi, Menejimenti inaomba idhini ya kuajili walinzi kutoka kwenye kampuni ya ulinzi ambapo kituo cha Afya Bugalama kitalindwa na mlinzi mmoja wa usiku, na wakati wa mchana Serikali ya kijiji itahusika na ulinzi huo. Kituo cha Afya Ibisabageni walinzi wawili (2) watakao linda usiku na mchana kwa kupokezana.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kushauri kutokana na mazingira ya vituo hivyo waajiriwe walinzi wanne kwani ujenzi huu ni wa muda mfupi, Pia pamoja na utaratibu wa kuajiri walinzi hao jamii iendelee kukumbushwa kuwa inajukumu la ya kulinda mali zilizopo eneo husika. Vile vile, walishauri mchanganuo wa gaharama za walinzi hao uoneshwe.

**KUMB NA. 10/5/12/2021; MAOMBI YA MABADILIKO YA MATUMIZI YA FEDHA ZA NDANI ZITUMIKE KWENYE UJENZI WA VYOO SHULE 2 SHIKIZI**

Afisa Mipango (W) aliwasilisha taarifa akieleza Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilitenga shilingi 10,000,000 kwa kila Kata ili itumike kwa miradi ya maendeleo kwa Kata husika. Jumla ya shilingi 370,000,000 ilizotengwa kupelekwa kila Kata kwa kipindi cha robo ya kwanza na ya pili.

Halmashauri pia ilipata jumla ya shilingi 100,000,000 kujenga madarasa 5 katika shule 2 shikizi za Nyamikoma (shule ya Lwenge) na Kawe (shule ya msingi Lubanda). Fedha



CamScanner

hiyo ililetwa kwa ajili ya kujenga madarasa na kutengeneza madawati kwani shule hizo zinatakiwa kufunguliwa na kuanza kutoa huduma.

Kwa kuwa fedha ya mapato ya ndani ilipelekwa kwenye Kata na kwa kuzingatia mahitaji haya, Kata imeomba idhini ya kufanya mabadiliko ya fedha iliyotengwa awali zifanyiwe mabadiliko kama ifuatavyo

- Fedha iliyotengwa kwa ujenzi wa vyoo na vichomea taka zitokanazo na uzazi Zahanati ya Misri Kata ya Bugalama, zitumike kujenga matundu ya vyoo shule shikizi ya Nyamikoma.
- Fedha iliyotengwa kwa ajili ya kukamilisha maabara ya Zahanati ya Shilungule Kata ya Busanda zitumike kujenga vyoo shule shikizi ya Kawe.

Wajumbe walipokea taarifa husika na kutoa idhini ya kufanya mabadiliko ya matumizi ya fedha kama ilivyoombwa kutoka Kata husika.

**KUMB. NA. 11/5/12/2021: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Katika kujadili mengineyo yafuatayo yalijitokeza:-

I. Kuhusu mabadiliko ya ratiba ya vikao wajumbe waliomba taarifa zitolewe kwa wakati na kila mjumbe apatiwe taarifa; na

II. Wajumbe walitoa shukrani za dhati na pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais SAMIA SULUHU HASSAN Rais wa awamu ya sita Kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa ya UVIKO 19.

**KUMB. NA. 12/5/12/2021; KUFUNGA KIKAO:**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao, ambapo kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti alisisitiza kuwa maazimio ya wajumbe yafanyiwe kazi kwa wakati.

Baada ya kusema hayo Mwenyekiti alifunga kikao saa 1:30 jioni.

**UMETHIBITISHWA**

**KATIBU** ................................ **MWENYEKITI** ................................

**TAREHE** 18.01.2022 **TAREHE** 18.01.2022